# STANDARD 8 KISWAHILI MID-TERM 1 2020

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA
## SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1-50, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali: Chagua jibu sahihi kutokana na maagizo uliyopewa**

**19.** Kamilisha kwa kiunganishi sahihi

*Kwetu kuna kila kitu __________ Meli.*

A. ingawa
B. ila
C. sembuse
D. wala

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

16. [A] [B] [C] [D]  17. [A] [B] [C] [D]  18. [A] [B] [C] [D]  19. [A] [B] [C] [D]

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Zoezi___1___kifungukate___2___kupima uwezo wa mwanafunzi kusoma na kufahamu habari___3___. Mwanafunzi___4___yafaa akumbuke kuna mada___5___zinaweza kutahiniwa katika sehemu hii. Vivumishi ni mojawapo ya sehemu___6___. Mfano wa vivumishi ni___7___.

1. **A.** ya **B.** za **C.** cha **D.** la
2. **A.** hukadiria **B.** hukusudiwa **C.** huthaminiwa **D.** huhusidiwa
3. **A.** aliopewa **B.** ililopewa **C.** alizopewa **D.** iliyopewa
4. **A.** yeyote **B.** yoyote **C.** zozote **D.** oote
5. **A.** mingi **B.** nyingi **C.** vingi **D.** zingi
6. **A.** inayotahiniwa **B.** linayotahiniwa **C.** zinazotahiniwa **D.** itahiniwayo
7. **A.** ghali, vichache, warembo, sugu, jema **B.** vyema, vibaya, kimoyomoyo, njiani **C.** katika, kwenye, ndani ya, juu ya **D.** Lo!Huree!Mama we! Jamani!Do!

Asubuhi___8___nilirauka na kutayarisha___9___.___10___kwa kuwa lazima ningeharakisha. Ninacho kumbuka ni kuwa, aila yangu___11___katika___12___ufukara usio na kifani. Ufukara huu ulitokana na kupigwa kalamu kwa baba yangu. Hata hivyo___13___. Mama yangu aliweza kuajiriwa katika kiwanda cha___14___nguvu za umeme. Ajira hii___15___kulipa pango tu bali pia karo yetu sote tuliokuwa shuleni.

8. **A.** huo **B.** hilo **C.** hicho **D.** hiyo
9. **A.** staftahi **B.** kilalio **C.** kijio **D.** chamchana
10. **A.** Nilichana mbuga **B.** Nilienda pecha **C.** Nilitia nanga **D.** Nilipiga miludi
11. **A.** tulikuwa tumezama **B.** walikuwa wamezama **C.** ilikuwa imezama **D.** lilikuwa limezama
12. **A.** biwi la **B.** lindi la **C.** shuke la **D.** tita la
13. **A.** Mungu akiziba hapa huzibua pale **B.** hakuna marefu yasiyokuwa na ncha **C.** Mungu hufufua nyama kitangani **D.** hakuna ziada mbovu
14. **A.** kutoa **B.** kuzaa **C.** kutengeneza **D.** kuzalisha
15. **A.** ilimwezesha **B.** haikumwezesha **C.** lilimwezesha **D.** ulimwezesha



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Chagua sentensi yenye kiambishi **-ki-** cha kuonyesha kuendelea kwa kitendo

A. Mutiso alikichukua jana asubuhi.

B. Mgonjwa akihudumiwa mapema atapona.

C. Mgeni huyo alikuwa amevalia kitamaduni.

D. Wamekuwa wakijiandaa tangu asubuhi.

**17.** Chagua sentensi iliyo katika hali timilifu

A. Wanafunzi huja shuleni kuelimika.

B. Angesoma kwa bidii angefaulu katika mtihani.

C. Mgeni atakapowasili tutamlaki.

D. Ufa umezibwa na mwashi.

**18.** **Ni nini maana ya sentensi hii**

*Yohana angalifuata maagizo asingalikanyaga chechele*

A. Alifuata maagizo na kukanyaga chechele.

B. Kutofuata maagizo kulimfanya asikanyage chechele.

C. Hakukanyaga chechele maadamu alifuata maagizo.

D. Alikanyaga chechele kwa kukaidi maagizo aliyopewa.

**19.** Kutokana na kitenzi **'cheka'** tunapata kivumishi

A. Mcheshi.

B. Kicheko.

C. Ucheshi.

D. Kuchekesha.

**20.** **Kanusha sentensi ifuatayo:**

*Ukuta uliopasuka umekarabatiwa*

A. Ukuta haukupasuka wala kukarabatiwa.

B. Ukuta uliopasuka haujakarabatiwa.

C. Ukuta usiopasuka haujakarabatiwa.

D. Ukuta usiopasuka haukukarabatiwa.

**21.** Sentensi ifuatayo imetumia tamathali gani ya usemi?

*Ikonya anaweza kuandika insha kurasa kumi kwa dakika moja*

A. Chuku.

B. Jazanda.

C. Sitiari.

D. Nahau.

**22.** **Andika udogo wa**

Mto huo ukikauka ng'ombe wetu watafariki.

A. Vijito hivi vikikauka vigombe vyetu vitafariki.

B. Kijito hiki kikikauka ng'ombe wetu atafariki.

C. Kijito hiki kikikauka vigombe vyangu vitafariki.

D. Kijito hiki kikikauka vigombe vyetu vitafariki.

**23.** Ni kundi lipi lenye vielezi pekee?

A. Cheupe, kipya, kizuri, kingine.

B. Sana, haraka, zaidi, vizuri.

C. Tena, rahisi, bora, haraka.

D. Keti, kunja, eleza, amua.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

24. Chagua mdudu asiyeambatana na wengine

A. Kipepeo.

B. Mbu.

C. Mbung'o.

D. Kiroboto.

25. **Tegua kitendawili**

*Kutwa nzima anashinda akipepeta na usiku kupumzika*

A. Kope.

B. Moyo.

C. Jua.

D. Pua.

26. **Chagua kiwakilishi**

*Wengine wakienda leo watahudumiwa tu*

A. wakienda.

B. wengine.

C. tu

D. leo

27. Ni sentensi ipi ambayo ina 'O' rejeshi tamati?

A. Kikulacho ki nguoni mwako.

B. Shambani walipolima pana magugu mengi.

C. Mwanariadha aliyetuzwa medali ya dhahabu alifurahi sana.

D. Wanafunzi waliofuzu katika mtihani huo ndio watajiunga na kidato cha kwanza.

28. Majina yafuatayo yako katika ngeli gani?

*Mazingira, mate, marashi*

A. U - ZI

B. U - YA

C. U - U

D. YA - YA

29. Mshororo ufuatao una mizani mingapi?

*Usipouziba ufa, utaujenga ukuta.*

A. 8

B. 16

C. 9

D. 18

30. Ikiwa mtondogoo itakuwa jumatatu, leo ni

A. Alhamisi.

B. Ijumaa.

C. Jumatano.

D. Jumanne.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.*

Hapa nchini Kenya, tuko na uraibu wa aina mingi. Sigara ni mojawapo ya uraibu ambao watu wengi sana wanashiriki. Kila uchao vijana hujitosa katika uraibu huu hatari kwa kujua au kwa kutojua. Wengine ni rubaa huwashinikiza ili waweze kukubalika katika tabaka au kundi fulani. Tuko na wengi ambao hawafahamu madhara ya sigara kwa vile huwa hayako wazi. Madhara yake huchukua muda mrefu kabla ya kuonekana au kudhihirika. Yanapofika kiwango hiki, mvutaji huwa amefikia uharibifu wa viungo vya ndani kwa hali ya juu. Kwa vijana hawa mguu mmoja huwa duniani na huo mwingine kaburini.

Sigara husheheni kemikali zaidi ya elfu kadhaa. Nyingi za kemikali hizi ni hatari na hudhuru. Hizi ni pamoja na nikotini, hewa ya kaboni monoksaidi na lami. Kemikali hizi huingia mwilini kupitia kwa mapafu na ***kufanya mili kuingia ufu***. Baadhi ya maradhi ambayo husababishwa na uvutaji sigara ni pamoja na maradhi ya kansa, vidonda vya tumbo na shinikizo la damu. Shinikizo hili linaweza kuleta maradhi ya moyo na kupooza kwa mwili.

Moshi wa sigara nao unapovutwa mwilini huingia na kugandama katika kingo za mapafu kama lami. Lami nayo huwa na sumu kali inayoweza kuharibu mapafu. Umio nao unafanywa kuwa mwembamba na sumu hii. Hii husababisha kuweko kwa unyevu unaolandana na kamasi. Ni vyema kujua kuwa hata kupumua moshi wa sigara hudhuru afya yako.

Ninatoa wito kwa akina mama wajawazito waambae sigara kwa vyovyote vile. Sigara inaweza kuharibu mimba ama ikafanya mtoto akazaliwa kabla ya wakati wake kutimia. Aidha, anaweza kuzaliwa akiwa na uzani wa chini sana. Mtoto kama huyu huwa na kinga ya chini sana.

Usidhani kuwa watengenezaji wa sigara hawajui madhara yake. Kwa kuzingatia hili, onyo hutolewa kwenye pakiti za sigara kuwa uvutaji wa sigara una madhara kwa afya ya mvutaji. Hata hivyo wavutaji wengi huwa hawatilii maanani maonyo na tahadhari hizi. Lakini kwa kuwa haja yao kubwa ni pato, bado huimarisha utengenezaji wazo. Si ajabu kusikia kuwa ni hatia kuuza sigara katika baadhi ya nchi hasa zile zilizoendelea.

Zile kampuni ambazo hutengeneza sigara huwa na hila sana. Kama umewahi kuona matangazo hutolewa kwa njia nyingi za mawasiliano kama vile runinga, redio na magazeti. Nayo hunadi starehe kuu kwa wavutaji. Kwa kuwa wanajua athari za sigara, huweka onyo pembeni pa pakiti kwa maandishi madogo sana yasiyoonekana vyema wala yasiyovutia makini ya watu.

***Ni jambo la kushangaza kuona kuwa, kampuni za sigara ndizo zinazoongoza katika kuelimisha vijana kuhusu madhara ya sigara***. Kuna uwezekano mkubwa kuwa hii ni mbinu ya kuwahamasisha vijana kuhusu kuwepo kwa bidhaa zao ili wawe wateja wa siku za usoni.

Taifa la Kenya, hupata ushuru mkubwa sana kutokana na mauzo ya sigara. Viwanda vya sigara huwaajiri maelfu ya vijana wasio na ajira. Vijana hawa wakipata ajira hawatafikiria kutenda uhalifu wowote kwa kuwa kila wakati watakuwa wakijishughulisha. Lakini ukweli ni kuwa uvutaji wa sigara una madhara mengi sana.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
A. sigara ndio tu uraibu wa pekee ambao unatumiwa na vijana.
B. vijana wote wanaovuta sigara wanajua kuwa ziko na madhara.
C. kuna baadhi ya vijana wanaovuta sigara kwa kushinikizwa na vijana wenzao.
D. njia ya pekee ya kukubalika kuwa kijana ni kuvuta sigara.

**32.** Vijana ambao mguu mmoja uko duniani na huo mwingine kaburini huwa
A. katika hali ya mahututi.
B. katika hali ya majuto.
C. katika hali ya maumivu.
D. Katika hali ya kilio.

**33.** ***Kufanya mili kuingia ufa***. Hii inafanya mili
A. kuharibika.
B. kufa.
C. kupata matatizo.
D. kubadilika.

**34.** Kulingana na aya ya tatu
A. moshi wa sigara ukivutwa, hubadilika na kuwa lami.
B. uvutaji wa sigara humfanya mtu kupenya kamasi mara kwa mara.
C. uvutaji wa sigara unaweza kusababisha shinikizo la damu.
D. hata mtu asiyevuta sigara anaweza kuathiriwa na anayevuta

**35.** Zifuatazo ni athari za sigara kwa mama mjamzito ila uvutaji wa
A. sigara inaweza kusababisha mtoto akazaliwa kabla ya wakati wake kufika.
B. sigara inaweza kumfanya mtoto kupunguza uzazi sana.
C. sigara hupunguza kinga ya mtoto.
D. sigara huimarisha afya ya mtoto kabla ya kuzaliwa.

**36.** Watengenezaji wa sigara
A. huwa hawajui madhara ya sigara.
B. wanajua madhara ya sigara.
C. huenda hawajui madhara ya sigara.
D. hawakuzi tumbaku mashambani mwao.

**37.** Kulingana na aya ya sita
A. kampuni za kutengeneza sigara huwa zimedhamiria kuwafahamisha wavutaji kuhusu athari za uvutaji wa sigara.
B. kampuni za sigara huwa zimelenga faida na si athari za uvutaji.
C. kampuni za utengenezaji wa sigara huwa zina haja sana watu wajue athari za uvutaji wa sigara.
D. Wavutaji wengi wa sigara huwa hawasomi maandishi yaliyoko kwenye pakiti.

**38.** *Ni jambo la kushangaza kuona kuwa kampuni za sigara ndizo zinazoongoza katika kuelimisha vijana kuhusu madhara ya sigara*. Taja tamathali ya lugha iliyotumika katika kauli hii
A. Chuku.
B. Istiara.
C. Tashbihi.
D. Kinaya.

**39.** Ni kweli kusema kuwa
A. sigara zina faida kubwa nchini.
B. sigara hazina faida yoyote.
C. sigara zina hasara pekee.
D. sigara hazisaidii kwa chochote.

**40.** Njia moja ya kupunguza uhalifu nchini ni
A. kuruhusu vijana wavute sigara.
B. kuwataka vijana wote wapate elimu ya juu.
C. kuwataka vijana waache kuvuta sigara.
D. kubuni nafasi za kazi kwa vijana.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Chaurembo alipokuwa katika shule ya msingi alifunzwa kuwa na maadili. Licha ya kuwa akili zake zilikuwa butu, walimu walijikaza kumfunza kwa njia ambayo ilistahili. Kumbe si masomo tu alikuwa haelewi. Uchafu wa mawazo alikuwa akiukumbatia vilivyo. Hata nyumbani hakuzingatia maonyo ya wazazi wake. Yaliingilia sikio moja na kutokea jingine.

Ajabu huajabiwa Chaurembo alipomaliza masomo ya shule ya msingi, alikutana na mwanamume mmoja kwa jina Bwana Tamaa. Alikuwa tajiri wa mali. Bwana Tamaa alindaganya Chaurembo akadanganyika. Kutokana na haya, Chaurembo alitoroka kwao na kwenda kwake. Kumbuka Bwana Tamaa alikuwa amewataliki wake wawili. Basi Chaurembo akawa mke mlezi. Ikabidi awalee watoto waliobaki na baba yao baada ya mama zao kusanzuka. Awali, Chaurembo alifurahia ingawa aliona aibu kuitwa mama kabla ya kumkopoa mtoto wake mwenyewe. Aliwabeza waliokuwepo awali na akajiona kuwa yeye ndiye aliyekuwa mchukizi bora. Akadharau na kusema kuwa pakacha likivuja nafuu huwa ni kwa yule mchukuzi. Hapo akaanza kuwaona wenzake kama maua yaliyonyauka ilhali lake ndilo kwanza lilikuwa likionana na jua.

Baada ya muda mfupi, alikuwa tayari mama wa watoto watatu. Mumewe naye hakutulia. ***<u>Alikuwa na jicho la nje</u>***. Akaimarisha nyendo zake za kiguu na njia. Chaurembo hangeenda kokote. Tayari alikuwa mlezi wa watoto wake na wasio wake. Vijisenene senene vikaongezeka. Lakini alivumilia akidhani angezila mbivu. Lakini wapi? Alipoligema ilibidi alinywe. Siku hazigandi. Chaurembo akajuta kwa kutowasikiliza wakuu na kukimbilia makuu. Pesa alizozikimbilia akawa anazisikiliza kama hadithi ndotoni. Kwao nako kukawa hawezi kurudi alipojipata amehimili ujauzito wa nne. Kama kawaida aliendа katika kliniki. Alipopimwa alipatikana na ugonjwa wa ukimwi. Mtoto alipozaliwa akaaga dunia. Naye Bwana Tamaa akaanza kumnyanyasa.

Baada ya muda mfupi, Bwana Tamaa aliyekuwa akijitapa kwa unene na mali akaanza kupotelewa na kiriba chake cha tumbo. Homa za hapa na pale zikaanza kumnyemelea. Vipelevipele vikaanza kusambaa mwilini. Alianza kusema kuwa Chaurembo alimwambukiza ugonjwa wa ukimwi. Lakini waliokuwa pembe za chaki walijua ukweli ulipokuwa. Baadhi ya vidosho wake walianza kupukutika kama majani. Isitoshe walikuwa hoi kitandani wakiwa hawajijui hawajitambui. Pesa zikawaishia wakawa waya. Hatimaye Bwana Tamaa alitangulia mbele ya haki.

Si ndugu si marafiki hawakumwelewa Chaurembo. Walimwona kama pweza aliyejipalia makaa makubwa ya moto. Ada za shule zikawa ni shida. Huruma ikawaingia majirani. Wengi wakasema lisilobudi hutendwa. Wakaubeba mzigo kwa hiari yao. Wakaandaa mchango wa harambee. Mwishowe naye Chaurembo akaaga dunia. Hapo ikabidi watoto walelewe na wahisani.

Nao walimwengu wakaja kujua kuwa uzuri si hoja, hoja ni tabia. Ukimwi umemaliza familia nyingi. Basi jamii hiyo ikaapa kuwa wao hawangekuwa watumwa wa tabia iletayo ukimwi. Walitambua kuwa ukimwi hurudisha nyuma maendeleo na ni vyema kutahadhari kabla ya hatari.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Ni methali gani ambayo ***hailengi*** kifungu ulichokisoma
A. Tamaa mbele mauti nyuma.
B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
C. Mwisho wa tamaa ni tama.
D. Mzigo wa mwenzio ni ukanda wa usufi.

42. Chaurembo
A. aliachia masomo katika shule ya upili.
B. alikuwa mwerevu kuanzia darasa la kwanza hadi la nane.
C. hakuelewa masomo labda kwa ukaidi wake.
D. alipata mfadhili wa masomo yake ya shule ya upili.

43. Bwana Tamaa alikuwa mtu mwenye tamaa. Mwandishi ametumia mbinu gani ya uandishi?
A. Jazanda.
B. Majazi.
C. Nidaa.
D. Tashhisi.

44. Ni wazi kuwa, Chaurembo
A. alivutiwa na elimu ya juu ya Bwana Tamaa.
B. alivutiwa na utajiri wa Bwana Tamaa.
C. Alivutiwa na mlahaka mzuri wa Bwana Tamaa.
D. alipendenzwa na umbo la Bwana Tamaa.

45. ***Alikuwa na jicho la nje***. Yaani
A. alikuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa.
B. alikuwa na hasira nyingi katika ndoa.
C. alipenda sana kutibiwa macho kutokana na kutembea sana.
D. alipenda kuoa bibi mwingine ili awe na familia kubwa.

46. Kilichomfanya Chaurembo ashindwe kurudi kwao ni kuwa
A. wazazi wake hawangekubali arudi kwa kuwa tayari alikuwa ameolewa.
B. tayari alikuwa na watoto watatu na wa nne alikuwa njiani.
C. aliwatukana wazazi wake siku aliyoondoka kwao.
D. wazazi wake walikuwa tayari wamehama pale alipowaacha.

47. Zifuatazo ni njia za kuambukiza ugonjwa wa ukimwi ila
A. kutiwa damu ambayo haijakaguliwa.
B. mtu aliye na virusi vya ukimwi kujamiiana bila kinga.
C. damu ya mtu mwenye virusi vya ukimwi kutiwa mama mjamzito.
D. mtu mwenye virusi kutumia kikombe kimoja na wagonjwa wale wengine.

48. Chagua kauli iliyo ya kweli
A. Chaurembo ndiye aliyemwambukiza Bwana Tamaa Ugonjwa wa ukimwi.
B. Bwana Tamaa ndiye aliyemwambukiza Chaurembo ugonjwa wa ukimwi.
C. Watoto wote wa Bwana Tamaa walikuwa na ugonjwa wa ukimwi.
D. Majirani waliwatelekeza watoto wa Bwana Tamaa.

49. Ni nini hasa kilichosababisha vifo vya Chaurembo na Bwana Tamaa?
A. Ukimwi.
B. Mali.
C. Tamaa.
D. Chuki.

50. Funzo kutokana na kifungu hiki ni kuwa
A. Yote yang'aayo si dhahabu.
B. Kila wakati mali huingiza mtu katika taabu.
C. Ni vizuri kuolewa baada ya kukamilisha masomo.
D. Ugonjwa wa ukimwi huwafanya watoto kuwa mayatima.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com